# MAPENDEKEZO YA MABORESHO YA MFUMO WA MASOKO YA KAHAWA TANZANIA

Wizara ya Kilimo.

5 Aprili 2019

# UTANGULIZI

Serikali katika kuboresha usimamizi wa mazao ya kipaumbele katika msimu 2018/2019 ilifanya mabadiliko yaliyolenga kuimarisha vyama vya ushirika na kuvipa jukumu la;

- Kukusanya kahawa ya wakulima.
- kupeleka kahawa kwenye viwanda vya kukoboa na
- Kuuza kahawa kwenye masoko ya kahawa

# MAFANIKIO YA MFUMO

Mfumo umeonekana kuwa na mafanikio kama vile;

- Takwimu za wakulima na uzalishaji wa kahawa kupatikana kwa usahihi.
- Kupungua kwa kahawa inayouzwa katika mfumo usio rasmi
- Kuimarika kwa ubora wa kahawa
- Kuweza kupanga  mipango ya maendeleo

# MAFANIKIO YA MFUMO

- Kuwezesha wakulima kupungaza gharama za uzalishaji kwa kuagiza pembejeo kwa pamoja

- Kuwezesha serikali za mitaa na serikali kuu kupata mapato yake kulingana na uzalishaji.

- Wakulima kuwa na nguvu ya kujadili bei (bargaining power)

# CHANGAMOTO

Pia utekelezaji wa mfumo huu mpya ulikuwa na changamoto zifuatazo;

- Kushuka kusikotarajiwa kwa bei ya kahawa katika soko la Dunia
- Kiasi kikubwa cha kahawa kuingizwa katika mnada mmoja kushinda mahitaji ya wanunuzi.
- Malipo ya awali kwa wakulima kuchelewa kutolewa kutokana na kahawa kuchelewa kupelekwa sokoni.

# CHANGAMOTO….

- Mahusiano kati ya wauzaji kahawa na makampuni ya nje ya kununua na kukaanga kuwa katika hali ya wasiwasi.

- Baadhi vya viwanda vya kukobolea kahawa kutokufanya kazi hasa vile vya makampuni binafsi

- Kuathirika kwa ubora wa kahawa ya Arabika kutokana na Ombwe la utaalam wa shughuli za kusimamia na kuendesha viwanda vya awali vya kuchakata kahawa (CPU)

# UBORESHAJI MFUMO WA MASOKO

- Kutokana na changamoto zilizojitokeza Bodi ya kahawa ilipokea maelekezo ya kuboresho masoko ya kahawa yaliyotolewa na Mh. Waziri Mkuu ya kuanzisha minada katika maeneo ya uzalishaji.

- Ilielekezwa kuwa minada ya kahawa ianzishwe katika kanda zifutazo;

- Songwe) - Songwe,Mbeya, Katavi
- Kagera- Kagera, Kigoma Mara na Mwanza
- Ruvuma- Ruvuma, Iringa, Njombe
- Kilimanjaro- Kilimanjaro, Arusha, Manyara, T[illegible]ga Morogoro

Minada hii ya kanda ilitarajiwa kuwa na faida zifuatazo:

- Wazalishaji kahawa watashiriki na kuona utaratibu mzima, jinsi kahawa yao inavyouzwa

- Kupunguza tatizo la malipo ya wakulima kuchukua muda mrefu kutokana na utaratibu mrefu uliopo wa masoko ya kahawa
- Kutangaza sifa za kahawa zinazopatikana kutokana na mazingira ya uzalishaji (Appelation);

- Wazalishaji kahawa watapata mrejesho kwa njia rahisi na sababu zilizosababisha kupata bei waliyopata Mf. mapungufu ya ubora

- Kupunguza gharama za usafirishaji wa sampuli kwenda kwenye soko la kitaifa (Central Auction).

# UTEKELEZAJI WA MAAGIZO

Bodi ya Kahawa ilianza utekelezaji wa maagizo haya kwa kufanya yafuatayo

- kufanya uhamasishaji na kutoa ufafanuzi wa utaratibu mpya
- kupata maoni ya wadau
- Awali pendekezo lilikuwa minada ya kanda iwe ya kahawa ghafi ili kupungua muda wa malipo ya wakulima kutokana na mlolongo mrefu wa masoko ya kahawa

# Maoni ya kanda za Mbeya/Songwe na Ruvuma

Mahitaji yao ni minada ya kahawa safi na si ghafi kama inavyopendekezwa awali na walitoa

sababu zifuatazo:

- Kuuza kahawa ghafi kutawarudisha nyuma wakulima kwa kuwa watauza kahawa bila ya kuzingatia madaraja;
- Kuuza kahawa ghafi kunaweza kuongeza kiasi cha kahawa inayouzwa katika mfumo usio rasmi.
- Wakulima watatumia fursa hiyo ya minada kukutana na wanunuzi wa kahawa yao.
- Kupungua kwa gharama ya kusafirisha sampuli.

# Maoni ya wadau Kanda ya Kagera

Wadau wa kahawa wa kanda ya Kagera walipendekeza kuwa minada inayotakiwa kufanyika kwenye kanda hiyo ni minada ya kahawa ya maganda,wakitoa sababu zifuatazo;

- Itapunguza muda wa malipo ya kahawa.
- Itapunguza gharama za usafirishaji wa sampuli
- Itaondoa hatari kwa mkulima inayotokana na kubadilika kwa bei ( Risk)
- Kutangaza sifa za kahawa inayopatikana kutokana na mazingira ya uzalishaji.

# UCHAMBUZI WA MAONI

Baada ya kupata maoni hayo ya wadau, tathmini ya mifumo mbalimbali ya masoko ya kahawa iliyopo nchini ilifanyika kama ifuatavyo:

# MINADA YA KANDA( Kahawa Ghafi)

- Faida
  - Kufupisha muda wa malipo ya wakulima
  - Kupunguza gharama za kuongeza thamani
  - Kumuondolea mkulima risk zitokanazo na tabia ya masoko ya kahawa
  - Kupanua wigo wa wawekezaji wenye viwanda kupata malighafi
- Changamoto
  - Kukosa manufaa ya bei inayotokana na ubora
  - Uwezekano wa kuchochea biashara isiyo rasmi

# MINADA YA KANDA( Kahawa Safi)

Faida

- Kupunguza gharama za usafirishaji sampuli
- Kuongeza ushiriki wa wakulima kwenye minada, hivyo kupunguza malalamiko kuwa wanaibiwa
- Kuongeza fursa za biashara na uwekezaji

# MINADA YA KANDA ( Kahawa Safi)

**Changamoto**

- Kupunguza kiwango cha kahawa kinachopatikana sokoni kwa sababu kiasili kahawa huiva kwa viwango tofauti,.
- Kuongeza gharama za uendeshaji kwa wanunuzi kahawa kwa kuwa yatalazimika kufungua ofisi za uendeshaji katika  kila maeneo ambayo mnada utaendeshwa.
- Kupungua kwa aina ya bidhaa zinazopatikana sokoni
- Kuongezeka kwa gharama za kuendeshea minada kwa kuwa itahitajika kujenga maabara za kutathmini ubora wa kahawa katika maeneo ya uzalishaji zenye kukidhi viwango vya kimataifa;

# MINADA YA KANDA ( Kahawa Safi)

- Kuongeza gharama za utunzaji kahawa kwenye maghala ya bandarini kwa kuwa upatikanaji wa mzigo ni kidogo kidogo.
- Idadi ya wanunuzi wakubwa wanaonunua kahawa mnadani (*Coffee Traders*) ni wanne, hivyo itawawia vigumu kuhudhuria minada yote hivyo kuanza kutumia watu wa kati (middlemen) kwenye kununua kahawa;
- Kupungua kwa bei ya kahawa kutokana na kuongezeka kwa gharama za kufanya biashara kwa kuwa wanunuzi watalazimika kusafiri kila eneo la mnada kununua kahawa
- Muda uliobaki kabla ya msimu mpya kuanza hautoshi kwa wanunuzi kufanya maandalizi ili kushiriki katika minada kikamilifu.

# MNADA WA KITAIFA(CENTRALIZED AUCTION)

- Faida
  - Wanunuzi wanaweza kupata kahawa ya nchi nzima katika eneo moja.
  - kuongeza utambuzi wa bei (price discovery).
  - Ni soko rejea (reference market) kwa vyama vya ushirika na wazalishaji wengine wa kahawa.
  - Kutangaza kahawa za Tanzania.
  - Kuimarika kwa mfumo wa upatikanaji wa takwimu za uzalishaji na mauzo ya kahawa.
  - Kahawa inauzwa ikiwa katika maeneo ya uzalishaji.

# MNADA WA KITAIFA (CENTRALIZED AUCTION)

- Changamoto
  - Gharama za sampuli.
  - Ushiriki mdogo wa wakulima kwenye mnada (physical presence).
  - Wanunuzi wachache.
  - Utaratibu mrefu wa malipo.

# SOKO LA BIDHAA (TMX)

- Faida
  - Unaendeshwa katika mfumo wa kisasa.
  - Mfumo wa uendeshaji wa soko hili hauna tofauti sana na uendeshaji wa mnada wa kahawa wa sasa wa Kitaifa.
  - Uwezekano wa kuwashirikisha wakulima katika maeneo ya kanda (price tickers).
  - Kuna uwezekano wa kuongeza idiadi ya washiriki wa mnada kupitia ushiriki wa kimtandao.
  - Kupunguza muda wa malipo kwa kutumia mfumo wa T+1.

# SOKO LA BIDHAA (TMX)

- Changamoto
  - Mfumo haujawa tayari, matarajio ni kwamba TMX itatumia mfumo wa sasa wa uendeshaji wa minada katika kipindi cha mpito.
  - Mfumo mpya unaohitaji elimu na uhamasishaji (capacity building) kwa wadau.

# SOKO LA MOJA KWA MOJA ( DIRECT EXPORT)

- **Faida**
  - Kuwepo kwa mahusiano ya kibiashara kati ya wazalishaji na wanunuzi wa kahawa.
  - Inatoa bei nzuri kulinganisha na bei ya mnada.
  - Uhakika wa soko na bei kwa muda mrefu.
  - Ubora wa kahawa ya Tanzania.
  - Ufuatiliaji wa kahawa kutoka kwa mnunuzi (traceability).

# SOKO LA MOJA KWA MOJA (DE)

- Changamoto
  - Kukosekana kwa uwazi katika makubaliano
  - Wakulima wadogo kushindwa kutekeleza wajibu wa kimikataba pindi bei zinapobadilika.
  - Utegemezi wa makampuni binafsi na mawakala kupata mikataba.
  - Kutimiza viwango vya juu vya ubora vinavyohitajika.

# SOKO LA VIWANDA VYA KUSINDIKA (INSTANT COFFEE)

**Faida**

- Kupata bei nzuri kutoka na kuongeza thamani
- Kusaidia ukuaji wa viwanda na hivyo kuongeza ajira na mapato.

**Changamoto**

- Soko dogo kutokana na uchache wa viwanda
- Uwezekano wa kuchelewa malipo ya wakulima kutoka na utaratibu mrefu

# MAPENDEKEZO YA MFUMO 2019/2020

Kutokana na uchambuzi huo mapendekezo ya kuboresha mfumo wa masoko ya kahawa ili uwe kama ufuatavyo:

# KUBORESHA SOKO LA MOJA KWA MOJA (DIRECT EXPORT)

Inapendekezwa kuwa kiasi kikubwa iwezekanavyo cha kahawa kiuzwe katika mfumo wa Soko la moja kwa moja kwa utaratibu wa ***forward sale*.**

Mfumo huu utafanya kazi kama ifuatavyo;

- Makubaliano yataingiwa kati ya wanunuzi wa kahawa na vyama vya ushirika chini ya usimamizi wa serikali.

# Soko la moja kwa moja…

- Makubaliano hayo yatahusisha upangaji wa bei kutokana na ubora na mwenendo wa bei kwenye soko la dunia.

- Makubaliano yanaweza kufikiwa hata kabla ya kahawa kuvunwa.
- Mnunuzi wa kahawa atatakiwa kuwezesha shughuli mbalimbali ikiwemo malipo ya awali ya kahawa( prefinancing), shunguli za ugani, ubora n.k

# Soko la moja kwa moja…

- Bodi ya kahawa itasimamia kuhakikisha makubalino yanatekelezwa.

- TCB itatoa cheti cha kuthibitisha ubora wa kahawa
- Pia wazalishaji wengine wenye masoko maalum wataruhusiwa kuuza kahawa yao ya madaraja yote kwenye mfumo wa DE

# 2. MINADA YA KAHAWA YA KANDA (KAHAWA GHAFI, KAHAWA SAFI)

Bodi ya Kahawa itaendesha minada ya kahawa ya kanda kwa kuuza kahawa safi kwenye kanda za

- Mbeya/Songwe,
- Ruvuma
- Kaskazini ( Kilimanjaro)

Minada ya kahawa ghafi (Dry Cherries) kwa kahawa ya kanda ya ziwa (Kagera) **Katika maeneo yatakayotangazwa.**

# 3. MNADA WA KITAIFA

- Mnada wa kitaifa utaendelea na utaendelea kufanyika kuuza kwa taratibu zilizopo wakati taratibu za kuhamishia mauzo ya kahawa kwenye soko la bidhaa (TMX) zikiendelea.

- Mara taratibu za kuhamishia mauzo ya kahawa kwenye soko la TMX zikikamilika pia wataendesha minada ya kanda,

- Bodi ya Kahawa itabaki na kazi yake ya msingi ya usimamizi.

# HITIMISHO

- Serikali inaamini kuwa mifumo hii pendekezwa itapunguza changamoto za masoko zilizojitokeza katika msimu wa 2018/2019

- Mifumo hii imezingatia matakwa ya wadau wa kahawa nchini na hivyo kuweka wigo mpana zaidi wa masoko ya kahawa nchini.

- Katika mfumo huu vyama cha ushirika havitabanwa kuuza kahawa kwenye aina moja ya soko, chama husika kitatafakari na kuamua soko lenye tija kwa mauzo ya kahawa za wanachama wake.

# ASANTENI SANA